Wasaidizi Ustawi Wa Jamii Awamu Ya Pili:

Stadi zinazotumika kuwasaidia watoto waishio katika mazingira Hatarishi na familia zenye mahitaji maalumu

Siku ya 2

Taarifa mpya kuhusu VVU/UKIMWI

HIV/AIDS Update

Muhtasari

Mapitio Ya Siku

Malengo

1. Kuongeza stadi zinazohitajika katika kuwasaidia watoto na familia zilizo katika mchakato wa kuwa wazi kueleza kuwa wameathirika na UKIMWI
2. Kuongeza stadi zinazohusika na kutetea watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, familia na jamii/jumuia zao.
3. Kuongeza ujuzi/ufahamu juu ya (wa) kuzuia VVU na tiba
   - Matibabu -kwa watoto, vijana na watu wazima
   - Kuzuia maambukizi ya mama kwa mtoto PMTCT
   - Kuzuia kuambukiza wengine(Mazuio ya upili)Preventing Transmission to Others (Secondary Prevention)
   - hatari za matibabu ya muda mrefu(Long term treatment effects
4. Kuongeza ufahamu kuhusu hatari zinazowapata watoto walioathirika na kuathiriwa na VVU.

Malengo Ya Mafunzo-Endelea

5. kuendeleza stadi zinazoshughulika na utatuaji matatiz o ya kupunguza hatari za VVU zitakazotumiwa na vijana na vijana wa umri mkubwa
   - Kuzuia hatari na migogoro ya kijinsia (Reducing sexual risk and violence)
   - Kuzuia hatari zinazohusiana na utumiaji dawa za kulevya na ulevi mwingine
6. kuendeleza stadi zinazohusika na kutatua matatizo ya watoto na vijana katika maeneo ya afya ya akili, elimu na kutengeneza kipato (income development)
7. Kuongeza elimu kuhusu maswala ya matunzo nyumbani yanayohusu VVU kwa watoto na familia.
8. kuendeleza elimu juu ya masuala ya mwisho wa kuishi kwa watoto na familia zilizoathirika na kuathiriwa na ukimwi

Yaliyomo Siku Ya 2:

Mapitio Ya VVU Kwa Wasaidizi Ustawi Wa Jamii

- ***Kuweka wazi maswala ya VVU***
  - Mizani ya kuweka uwazi
  - Kuweka wazi kwa watoto
  - Kuweka wazi kwa watu wengine
    - Wenzi wa maisha-Sexual Partners
    - Familia
  - Kuweka wazi kwa jamii
- ***Utetezi kuhusu masuala ya VVU***
  - Utetezi wa mtu binafsi
  - Utetezi katika familia
  - Utetezi katika ngazi ya jamii

Mada Siku Ya 2 Inaendelea

- Mapitio ya maswala ya tiba ya VVU
  - Kuzuia maambukizo ya mama kwenda kwa mtoto, watoto wachanga, Vijana waliobalehe na matunzo ya watu wazima wenye VVU
- Kuwatunza watoto walioathirika na VVU
- Kupunguza hatari kwa watoto wakubwa
  - Kupunguza hatari za Kujamiiana
  - Kupunguza hatari za kutumia madawa kwa watoto wakubwa.
- Kutatua matatizo ya VVU kwa watoto na familia zao
- Masuala ya matunzo majumbani kwa watoto na familia
- masuala yahusuyo mwisho wa maisha/uhai

Kuwa Muwazi : Kuwaeleza Wengine Hali Zao Kuhusu VVU

Jinsi Ya Kuwasaidia Wanaoishi Na VVU: Kuamua Kuwa Muwazi Kuhusu Hali Ya Maambukizi Ya VVU

- Nani aelezwe/ajulishwe?
- Ni wakati gani unaofaa kusema?
- Useme/ueleze nini?
- Mahali gani ni muafaka kusema/kueleza ?
- Utawezaje kueleza/kusema?

Mjadala mafupi wa maswali haya

Mjadala Katika Vikundi Vidogo : Kuwa Muwazi Kuhusu Hali Ya Maambukizi Ya VVU

Zungumza na jirani yako kwa dakika 5 kuhusu suala hili kisha toa maelezo katika majadiliano ya kundi kubwa

Una uzoefu gani kuhusu:

- Watu waishio na VVU kuwaeleza wengine?
- Kufahamu hali ya mtu mwenye VVU

Mzani Wa Uwazi Kuhusu VVU

- Watu hutofautiana kulingana na wale wanaowaeleza na kile wanachokisema
- Tunaweza kulitafakari suala hili kwa misingi ya kuanzia na kutomweleza mtu yeyote hadi kuwa wazi kuhusu hali ya VVU

Mzani Wa Uwazi Kuhusu VVU



Mzani Wa Uwazi Kuhusu VVU

- ***Mazoezi:***Wasimamishe washiriki wafanye/waonyeshe kwa vitendo kila hatua
- Jadilianeni kuhusu wanavyojisikia na pata maoni ya kikundi

Mzani Wa Uwazi Kuhusu VVU



Kushughulikia Siri

- Kutokuwa tayari kuwaambia wengine ukweli (au ukweli wote) kuhusu hali ya maambukizi ya VVU
- Kushughulika na hofu ya kukataliwa ambayo huathiri jinsi mtu anavyojisikia kuhusu yeye mwenyewe (ustawi wa binafsi)

Mzani Wa Uwazi Kuhusu VVU

- Yote kati ya haya ni sawa ilimradi ni uamuzi/uchaguzi wa mtu binafsi
- Msaidizi Ustawi wa Jamii anatakiwa kumsaidia mtu anayeishi na VVU ili kubaini anaweza kuwa wapi katika mzani na kwa sababu gani
- Ikiwa ataangukia upande wa usiri, msaidie mtu anayeishi na VVU kubaini/kutambua kama siri hiyo inamuumiza binafsi au kuwaumiza wengine
  - Watoto
  - Wenzi wa maisha
  - Wazazi na walezi wengine
  - Marafiki na wasaidizi wengine (walezi muhimu katika ukoo)

Ni Mazingira Gani Yanayofaa Ambayo Ni Muhimu Kueleza/Kusema Hali Ya VVU?

Bungua Bongo

Majadiliano Kuhusu Kuwa Muwazi Kuhusu Hali Ya VVU

- Kuna maswala gani kuhusu nani aambiwe au asiambiwe? Na maswala yanayohusiana ya “wakati gani” na “kwa namna gani”
- Kuna maswala gani katika kutoa matunzo ya muda mrefu na kupanga mipango inayohusu maswala ya VVU
  - Msaada wa familia kwa ajili ya matibabu
  - Kupanga mapema matunzo ya watoto na mgawanyo wa mali
  - kuwa muwazi kuhusu hali ya maambukizi ya VVU kwa lengo la kuzuia hali hatarishi zaidi
  - Kuna njia zipi zinazomwezesha Msaidizi Ustawi wa Jamiikuwasaidia watu wanaoishi na VVU kufanya maamuzi haya?

Mazingira Gani Yanafaa Kwa Ajili Ya Kueleza Hali Ya VVU

- Wenzi katika kujamiiana
- Watoa huduma za afya
- Watu wanaotoa huduma kwa wanaoishi na VVU/UKIMWI
- Watu wanaowahudumia watoto wa familia za waathirika
- Wanafamilia wengine na na watu wengine wa karibu wanaoaminiwa/wasiri wao,Wachungaji, viongozi wa kijamii n.k

Makundi haya yana maswala gani yanayofanana?

Kumsaidia Anayeishi Na VVU Au Mwanafamilia Kuamua Kuhusu Kueleza Hali Yake Ya VVU.

- Nani aelezwe/ajulishwe? (je tunawezaje kuamua?)
- Ni wakati gani unaofaa kusema? (mahusiano yanapokuwa yenye nguvu, kuhisi mhusika atalipokea, muda gani upite baada ya kubainika kuwa na VVU, n.k)
- Useme/ueleze nini? Muathirika anahitaji kuamua aeleze kwa kiasi gani – aeleze hali ya VVU tu au historia na hali ilivyo sasa, n.k
- Mahali gani ni muafaka kusema/kueleza
- Utaelezaje ?

Kuwasaidia Wateja? Namna Ya Kujiandaa Kueleza Hali Ya VVU

- Wakati wote ni uamuzi wa mteja kuhusu nani, nini, wapi, kwa namna gani na kwa nini kueleza
- Hakikisha kunakuwepo na usiri katika majadiliano yenu
- Tunaweza kusaidia kutafakari faida na hasara za kuwa muwazi kuhusu hali ya VVU
- Fanya mazoezi ya vitendo pamoja na mteja kuhusu hali ilivyo, iwe ni mzazi au mtoto– fanya mazozezi ya namna bora zaidi ya kutoa habari (buni mkakati na tafakari namna ya kuzishinda changamoto

Kwa Nini?– Ni Nini Sababu Za Kumweleza Mtu Na Hasa Kumweleza Sasa?

- ***Kushughulikia mahitaji yao binafsi na hofu zao:*** kupata ahueni baada ya kushirikisha siri zao
- Kwa sababu ni sehemu ya mahusiano
- Kwa sababu wanaanza kutumia za ART
- Kuepuka mtu kugundua hali ilivyo kutoka chanzo kingine
- Kuacha kuficha habari, matumizi ya dawa, n.k
- Kupata msaada kutoka kwa mtu kama mtoa huduma au msaada wao

Mambo Yanayojitokeza Baada Ya Kuwa Muwazi Kuhusu Hali Ya Maambukizi Ya VVU Kuhusu Hali Ya VVU Ya Mzazi Au Mtoto Kwa Mtoto

- Mto anafahamu nini?
- Je, mtoto mwenyewe anajua hali yake ya VVU?
- Ni nani amemwambia au hajamwambia?
- Ni kwa jinsi gani kuwa muwazi kuhusu hali ya VVU hutegemea hatua ya maendeleo/kukua kwa mtoto?
- Je, mtoto anajua hali ya VVU ya wanafamilia wengine?
- Nini jukumu la Msaidizi Ustawi Jamii?

Kuwa Muwazi Kuhusu Hali Ya VVU Kwa Mtoto

- Je hatua ya makuzi ya mtoto, huzuni na kupotelewa kunawezaje kuathiri uwazi wa mtoto kuhusu hali yake ya VVU
- Je kuna maswala gani mengine yanayohusu uwazi wa mtoto kuhusu hali yake ya VVU?
  - Afya ya mzazi na mpango wa kumtunza mzazi
  - Majadiliano kuhusu mipango ya baadaye kwa ajali ya mtoto
    - Matunzo,elimu,mali
  - Hali ya afya ya mtoto
- Je Kuna maswala gani maalumu kwa vijana wenye umri wa kwenda shule?
  - Makundi rika, ndugu aliozaliwa nao, marafiki maalum.
- Je ni kwa namna gani masuala uwazi kwa mtoto kuhusu VVU yanaweza kubadilika kulingana na wakati?

Kueleza Kulingana Na Kiwango Cha Uelewa Wa Mtoto.

- Umuhimu wa kutoa ujumbe kwa mtoto kulingana na kiwango cha hisia na uelewa wake
- Watoto wanaweza kujua VVU ni nini hata wakiwa katika umri mdogo
- Kujua kuwa mama anaumwa au alikufa kutokana na ugonjwa ni maelezo yanayotosha kwa watoto
- Kumsaidia mtoto kuelewa VVU ni nini na jinsi anavyowaathiri pindi mzazi au mwanafamilia mwingine anapokuwa na VVU au kufa kwa VVU/UKIMWI

Vipi Kuhusu Shule?

- Je mtoto yuko shule?
- Shule ina mtazamo au sera gani kuhusu VVU na wakina nani wanajua kuhusu VVU?
- Kuwa muwazi kuhusu hali ya VVU kwa wakurugenzi ,waalimu na wafanyakazi wengine?
- Vipi kuhusu kuwa muwazi kuhusu hali ya VVU kwa marafiki na wanarika?
- Wasaidizi Ustawi wa Jamii wanawezaje kusaidia?

Inakuwaje Kuhusu Jamii

- Mtoto anahusishwa katika shughuli/programu za jamii?
- Mtazamo au sera zao ni zipi na ni nani anajua kuhusu VVU?
- ***Msaidizi Ustawi Jamii atasaidia katika:***
  - Kutoa habari
  - Kutengeneza mpango
  - Kuwa kiungo kati ya familia na jamii

Majadiliano

- Tuambie shauri lolote ambalo umewahi kulishughulikia linalohusu maswala ya nani anajua kuhusu hali ya VVU?
- Tunawezaje kutoa msaada bora zaidi kwa watoto na familia ili waweze kuzitumia rasilimali zilizopo kwenye jamii?

Jadilini katika makundi makubwa au *katika vikundi vidogo* na kuleta mrejesho kwa kundi kubwa

Wajibu Wa Msaidizi Ustawi Wa Jamii Akiwa Mtetezi Wa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi Na Familia

Kuwasaidia Na Kuwauganisha Vijana Balehe Na Watoto Wanaoishi Na VVU

- Kupunguza hatari
- Kupima
- Matunzo na kusaidia
- Kutumia dawa za VVU
- Kuweka mpango kwa ajili ya vijanabalehe na watoto wanaoishi naVVU

Jinsi VVU/UKIMWI Unavyowaathiri Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi

- Watoto walio katika hatari yamaambukizi ya VVU—kujiingiza katika tabia hatarishi
- hatari na kupunguza hatari kwa vijana wakubwa na vijana balehe
- Watoto walioathiriwa wanaoishi na wanafamilia wenye VVU
  - Wazazi
  - Kaka/dada/Rafiki/Rafiki wa kiume/Rafiki wa kike
- Mtoto ambaye alikuwa na mzazi akafa kwa VVU(yatima kutokana na kupotelewa mzazi kwa ukimwi))
- Watoto wanaotunza wanafamilia/ ndugu walioathirika na VVU
  - Wazazi, Parents, Babu na bibi ndugu wa damu

Wmatoto Walioathirika Kwa KWA VVU/UKIMWI

- Jadili uzoefu wako katika kuwasaidia watoto walioathirika na UKIMWI
- Mahitaji yao ni yapi?

Bungua bongo

Kushughulikia Mahitaji Ya Watoto Walio Na Maambukizi Ya VVU

- Kuwa muwazi kuhusu hali ya maambukizi ya VVU na kupima kwa watoto wadogo
- Masuala ya matibabu yanayowahusu watoto
- Masuala ya kuzingatia tiba maalum kwa watoto
- Kupima,matibabu na kuzingatia tiba maalumu kwa vijana balehe.
- Masuala ya watoto na vijana balehe wanaoishi na VVU pamoja na matatizo mengine, ugonjwa na ulemavu
- Mpango wa muda mrefu kwa ajili ya watoto na vijanabalehe wanaoishi na VVU

Maswala Ya VVU Kwa Umri Na Ujinsia

Ni maswala yapi ya VVU yanahusiana na Umri na ujinsia

- Miaka 0-3
- Miaka 4 hadi 5
- Miaka 6 hadi 9
- Umri wa kabla ya kubalehe
- Umri wa kubalehe….

Jadili kwenye makundi makubwa au madogo

Watoto Walioathirika Kwa VVU/UKIMWI

- Upatikanaji wa madawa
  - Kutafuta na kuhakikisha kufikishwa kwao kwenye vituo vya afya na madaktari
  - Kuisaidia familia kuwasimamia watoto kutumia dawa kama ipasavyo
- Kutoa rasilimali ili kukidhi mahitaji mengine kusaidia huduma nzuri za afya na haki za msingi
  - Chakula , makazi, Mavazi, elimu na misaada mingine kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na familia zao

Dondoo Muhimu Kuhusu Kuzuia Maambukizi Toka Kwa Mama Kwenda Kwa Mtoto.

- VVU huambukizwa kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa mchakato wa kujifungua(kwa njia ya damu)
- Watoto wengi hawapati VVU wanapokuwa tumboni mwa mama zao
- Kujifungua ka upasuaji na kunawa sehemu za uke kunasaidia kupunguza maambikizi
- Maambukizi ya VVU wakati wa uchungu na kujifungua yanaweza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa kwa kuwatibu mama na mtoto mapema iwezekanavyo
- Mtoto anaweza kuambukizwa VVU wakati wa kunyonya kwa sababu virusi huishi kwenye maziwa ya mama na ni kwa sababu siku za kwanza za kunyonyesha mara nyingi chuchu huchubuka na huvuja damu.

Mabadiliko Ya Mwongozo Kuhusu Kuzuia Maambukizi Toka Kwa Mama Kwenda Kwa Mtoto. Januari 2011

- World Health Organization: http://www.who.int/pmtct http://www.who.int/child_adolescent_health/doc

Guidelines on HIV and infant feeding 2010: principles and recommendations for infant feeding in the context of HIV and a summary of evidence. **Geneva, World Health Organization, 2010. http://whqlibdoc.who.int/publications/ 2010/9789241599535_eng.pdf**

Mwongozo Mpya Wa Tiba Toka Shirika La Afya Duniani

1. Wakinamama wajawazito wote wenye VVU na seli damu (chini ya <350 CD4) wanapaswa waanze dawa mapema iwezekanavyo.
2. Wakinamama wote wajawazito wenye VVU na seli damu zaidi ya (>350 CD4) Mtoa huduma anapaswa kufikiria kuanza dawa lakini utaratibu wa tiba unaweza kuwa tofauti.
3. Watoto wote waliozaliwa na mama wenye VVU wanapaswa kunyonyeshwa kwa angalau miezi sita. Watoto wanaonyonyeshwa ni lazima wapate tiba ya kufubaza virusi kila siku kuanzia walipozaliwa hadi wiki 4 mpaka 6, au wiki1 baada ya kuacha kunyonya
4. Watoto wasionyonyeshwa wanapaswa wapewe dawa za kufubaza VVU hadi wanapoitimiza umri wa wiki 4 mpaka 6

Miongozo Ya Shirika La Afya Duniani Kwa Wakina Mama Waathirika Kuhusu Kuwanyonyesha Watoto

- Wakina mama ama wanyonyeshe na kutumia dawa za kufubaza virusi (ARVs) au waache kabisa kunyonyesha.
- ***Mahali ambapo kunyonyesha ni chaguo bora zaidi: Kunyonyesha miezi 6 bila chochote kingine, halafu aanzishiwe nyongeza ya chakula na aendelee kunyonya kwa miezi 12. Acha kunyonyesha taratibu na endelea kumpa dawa kwa wiki 1 baada ya kumwachisha kabisa Nyonyesha maziwa ya mama tu kwa miezi 6 ya mwanzo isipokuwa pale ambapo lishe mbadala ina kubalika,inawezekana, gharama inawezekana, ni endelevu na salama. (AFASS).***
- Ifikapo miezi 6,endelea kunyonyesha pamoja na kumpa chakula cha ziada iwapo kiwango cha AFASS hakijafikiwa Likiza katika kipindi cha siku 2-3 hadi wiki 2-3.

Matumizi Ya Dawa Za Kufubaza Virusi(ARV) Kwa Wakina Mama Wanaonyonyesha

- Mtoto anayenyonya na amezaliwa na mama mwenye VVU ambae anatumia ARV kwa ajili ya afya yake anapaswa , atumie Nevaripine kila siku au AZT mara mbili kwa siku kuansia anapozaliwa au mapema iwezekanavyo mpaka atakapofika umri wa wiki 4 hadi 6
- ***Watoto wanaopata chakula mbadala, na wazaliwa na wakina mama ambao wana VVU na wanatumia dawa za kufubaza VVU kwa ajili ya Afya zao, wanapaswa kutumia dawa ya NVP kila siku au*** AZT mara mbili kwa siku kuanzia siku anapozaliwa au mapema inavyo wezekana hadi atakapo fika umri wa wiki 4 hadi 6

Utafiti Uliofanyika Karibuni Kuhusu Maambukizi Kutoka Kwa Mama Kwenda Kwa Mtoto

- Uchunguzi wa wwakina mama na watoto huko Burkina Faso, Kenya na Africa ya Kusini(Kesho Bora Study)
- Mfumo wa Dawa tatu za -ARV huzuia maambikizi ya VVU kwa watoto kwa asilimia 43 na hupunguza hatari ya maambukizi kwa zaidi ya nusu wakati wa kunyonyesha
- Watoto waliozaliwa na wwakina mama ambao virusi havionekani kwa kipimo,(pungufu ya vijirudufu 50) kwa kutumia dawa za ARV ipasavyo hupunguza maambukizi kwa kiasi cha 2.7% wakati wa kuzaliwa mtoto kwa mwaka wa kwanza. Kwa hiyo ni muhimu kuanza ARV mapema wakati wa uja uzito, ikiwezekana kabla ya uja uzito

Reference: Kesho Bora randomized controlled clinical trial in fivesites in Burkina Faso, Kenya and South Africa.5th IAS Conference on HIV Pathogenesis,Treatment & Prevention. Cape Town, South Africa, 19–22 July 2009. Abstract LBPEC01. http://www.ias2009.org/pag/pdf/3631.pdf

Tafiti Mpya, Inaendelea…

- Unatoa matumaini mapya kwa wakina mama wenye VVU ambao hawawezi kutumia maziwa ya unga. Itaongeza nafasi ya mtoto kuendelea kuwa na afya na kutopata maambukizi kwa kuwa maziwa ya mama yana virutubisho vyote na humkinga mtoto dhidi ya magonjwa ya kufisha kama vichomi(pneumonia) na kuharisha
- Kuwapa kipaumbele cha kupima VVU na kupata dawa za ARV wwakina mama wajawazito na wanaopanga kubeba mimba itasaidia kuondoa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto
- wakina mama walio katika umri wa kuzaa wanahitaji msaada wa wasaidizi Ustawi wa Jamii ili kuelewa, kupata na kuzingatia matibabu

Kunyonyesha na Maambukizi ya VVU

- Katika miezi miwili ya mwanzo, mtoto anayenyonya kwa chupa yuko katika hatari ya kifo kwa kuharisha, magonjwa ya njia ya hewa au magonjwa mengine mara 6 zaidi ukilinganisha na mtoto anayenyonya ziwa la mama yake. Hii ni mara nyingi kwa sababu maji yasiyosalama hutumika katika kuchanganyia maziwa ya unga ,chupa hazina usafi wa kutosha matumizi ya chupa si salama na sababu nyinginezo.
- Usibadili kati ya maziwa ya mama na maziwa ya chupa kwenda mbele na kurudi nyuma kati ya maziwa ya mama na chupa.
- Endelea na matibabu ya mtoto wakati wa kumlikiza mwanzishie vyakula vingine taratibu.
- Kwa wakina mama VVU, wenye uwezo mdogo wa kupata maji safi na mazingira safi, mwongozo mpya, kuwatibu mama na mtoto wakati wa kunyonyesha itaondoa maumivu ya uchaguzi mgumu wa kunyonyesha ukiwa na VVU na kwa upande mwingine matumizi ya chupa na chakula kisicho salama

Msaidizi Ustawi Jamii Afanye Nini Ili Kumsaidia Mama Kuhusiana Na Ujauzito,Kujifungua Na Kumlisha Mtoto

Bungua bongo

Wasaidizi Ustawi wa Jamii, VVU na Ujauzito

- Wasaidie wakina mama kuwalinda watoto wao dhidi ya maambukizi
- Watie moyo wakina mama kutibiwa na dawa za VVU
- Toa unasihi kwa wakina mama kupanga ujauzito, kujifungua na kutunza watoto
- Kuwasaidia wakina mama wanaopata matibabu ya VVU kuzitegemeza familia zao ili kuhamasisha matunzo yanayohusiana na VVU
- Kutoa taarifa kuhusu unyonyeshaji salama na utunzaji mzuri wa watoto
- Fanya kazi na familia kusaidia wakina mama wenye VVU, watoto wao na familia zao

Wasaidizi Ustawi Wa Jamii, VVU Na Ujauzito,Inaendelea

- Kuisaidia familia, inapopitia kipindi cha kuwa na shinikizo mara mbili cha kujifungua na kugundulika kuwa na VVU kwa wakati mmoja. Hali mchanganyiko zenye ugumu familia inazopitia zinaweza kuibuka katika kipindi hiki cha shinikizo.
- Wasaidie watoa huduma za afya kuwasiliana maswala magumu ya ufahamu wa kitaalamu na mama pamoja na familia katika hali ambayo wote wataelewa kwa haraka.Muda ni muhimu sana.
- washauri wakina mama kupata dawa za ARV wakati wanaponyonyesha kwa ajili yao na watoto wao.
- Kuwasaidia wakina mama kupata huduma za matibabu ya matatizo ya matiti pamoja na vidonda au utandu(fangasi) mdomoni mwa mtoto

Wasaidizi Ustawi Wa Jamii Wanaweza Kufanya Nini Ili Kupunguza Maambukizi Ya Mama Kwenda Kwa Mtoto

- Wasaidia wanawake wajawazito kupimwa VVU na kupata dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARVs) ili kujiepusha na maambukizi, mapema iwezekanavyo.
- Wasaidie kutatua tatizo la upatikanaji wa fedha usafiri, uwezeshe upatikanaji wa huduma hizi
- Ikiwa hali zao zitagundulika wakati wa uja-uzito matibabu yaanze haraka iwezekanavyo kwa tiba yenye ufanisi.

Kuzingatia Matumizi Ya Dawa (Mapitio)

- ***Kuzingatia matibabu***:
  - maswala ya
    - Familia
    - Mtoto
    - maswala mengine ya watoa huduma kuhusu kuzingatia matibabu.
- Kwa nini kuzingatia matibabu ni muhimu?
  - Kuzuia kuendelea kwa ugonjwa
  - Kuzuia kuendelea kwa dalili za ugonjwa
  - Kuzuia maambukizi mengine
  - Kuzuia usugu wa dawa.

Mazingira Ya Huduma Za Matibabu Kwa Watoto

- Masuala maalumu ya kifamilia
- Masuala maalumu ya kijamii
- Kuzuia vikwazo vya ufahamu na elimu

Msaidizi Ustawi Wa Jamii Anawezaje Kuusaidia Mfumo Wa Tiba Uwasiliane Na Familia?

- ***Masuala ya mila/desturi na mtazamo wa jamii– wanaamini nini na shughuli zao za kila siku ni zipi au hawapati huduma za afya ndani ya jamii?***
- Mazingira ya familia
  - Hali ya kiuchumi
  - Hali iliyoathiriwa na magonjwa
    - Wazazi kuwa wazi kuhusu hali ya maambukizi ya VVU
    - kuwa wazi kuhusu hali ya maambukizi ya VVU mahususi kwa watoto

Kupunguza Hatari Ya Maambukizi Kwa Watoto: Hatari za Kujamiiana Na Hatari Nyinginezo.

Ni Hatari Zipi Zinaweza Kusababisha Maambukiz Ya VVU Kwa Watoto Wakubwa?

Bungua bongo

Kuna Hatari Gani Za Maambukizi Ya VVU Kwa Vijana?

- Tabia za ngono
  - Ngono zembe
  - Ngono katika umri mdogo
  - Magonjwa ya ngono ambayo hayakutibiwa
  - Ujauzito usiopangwa
  - Ngono ya hiari na ngono za kulazimishwa
  - Ngono kwa ajili ya kupata fedha au madawa ya kulevya
  - Kutumia vileo na kusababisha ngono zembe, ngono katika umri mdogo
- Kutumia sindano – kujidunga sindano za dawa za kulevya
- Others?

Hatari ya Ngono

- Je una uzoefu gani kuhusu watoto unaofanya kazi nao kuhusiana na VVU, hisia za ngono na tabia, nk.

(kwanza zungumza na jirani yako, halafu toa mrejesho katika kikundi)

Kujadili Ujinsia

- Tunajisikiaje kujadili masuala haya na vijana?

Mjadala Wa Ujinsia

- Jetunawezaje kujadiliana masuala haya na vijana?
  - Kwa kutumia lugha rahisi na ya moja kwa moja.
  - Kumuuliza mtoto kuwa anajisikia vizuri katika mjadala huu.
  - Kutumia wanarika kama rasilimali kwa ajili ya kuelimisha na kusaidia

Wasaidizi Ustawi Wa Jamii Wanawezaje Kupunguza Hatari Ya Maambukizo Kwa Vijana

Bungua Bongo

Masuala Ya Ujinsia Na Vijana

- Watoto wanapata taarifa za namna gani kuhusu masuala ya ujinsia ?
  - Kutoka kwa nani?
  - Katika umri gani?
  - Inajumuisha nini?
  - Kupunguza hatari?

Masuala Ya Ujinsia Katika Umri Tofauti

- Je hali hizi zinafana au kutofautio
  - Hisia za kimapenzi
  - Hisia za kufanya ngono
  - Tabia za ki ngono
- Je ni tabia gani za kingono unazoweza kujihusisha nazo?

Ni Lipi Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Kushughulikia…

- Ujinsia
- Madawa ya kulevya
- Hatari nyinginezo

Kupunguza Hatari Ya Maambukizi Ya VVU Kwa Watoto Wakubwa

- Je ni zipi baadhi ya njia za kupunguza maambukizi ya VVU?

Kupunguza Hatari ya Maambukizi Ya VVU Kwa Watoto Wakubwa

- Njia za kupunguza hatari za maambukizi ya VVU
  - Kuchelewesha tabia za kujamiiana
  - Shughuli zingine za kijamii
  - Kufanya maamuzi mazuri juu ya tabia za kujamiiana
    - Nini ni salama?
    - Nini si salama/hatari?
    - Jinsi gani ya kumua ?
  - Ulinzi
  - Kondom
  - Njia nyinginezo
  - Kusisitiza ujumbe

Habari za Ujinsia na Vijana….

- Utambulisho wa masuala ya ngono na ujinsia
- Unyanyasaji wa kingono
- Ngono kwa ridhaa dhidi ya ngono bila ridhaa (kutumia nguvu)
- Tabia hatarishi za kingono
- Ngono salama
- Kuzuia kubeba mimba
- Kupata msaada (Matibabu, Elimu na Habari, Unasihi)

Zoezi la Vikundi Vidogo darasani.

- Kufanya kazi katika vikundi vya watu 6
- Neema ni msichana mwenye umri wa miaka 12 anayeishi na babu yake, kwa kuwa wazazi wote wawili walikufa. Anaanza kuchelewa kurudi nyumbani hadi usiku wa manane na mara moja hakurejea nyumbani kabisa. Babu yake ana wasiwasi kuwa binti huyu ana marafiki wa kiume au ana mahusiano na wageni.

Darasani : Zoezi Katika Vikundi Vidogo

- Fanyeni igizo dhima fupi kuhusu unasihi na babu.Jadiliana na Neema kuhusu ngono au tabia hatarishi. au jadiliana na babu jinsi anavyoweza kuongea na kumsaidia Neema

Je Ni Kwa Jinsi Gani Msaidizi Ustawi Wa Jamii Anawezaje Kusaidia Kupunguza Sababu Hatarishi Za Ngono Kwa Watoto?

Kufanya ngono na mtoto,ama iwe ni kwa utashi au kwa kulazimishwa,ni unyanyasaji wa watoto kulingana na sheria ya Tanzania na kimataifa

- Je ni kwa Jinsi gani msaidizi Ustawi wa Jamii ataweza kusaidia kupunguza mazingira hatari ya ngono kwa watoto?
  - Je kuna mbinu tofauti zinazohitajika kwa vijana wadogo wa kiume au wa kike?
  - Ni kwa vipi uchumi hatarishi hupelekea kuanza ngono na hatari za mapema?

Utumiaji Vileo (Pombe, Dawa Zinginezo)

- Ni dawa gani ambazo vijana wanaweza kutumia? Je unayaona haya?

Utumiaji Vileo (Pombe, Dawa Zinginezo)

- Ni dawa gani ambazo vijana wanaweza kutumia? Je unayaona haya?
  - Tumbaku
  - Pombe
  - Bangi
  - “dawa za kulevya”– heroine, n,k.

  Inaweza kuhusisha matumizi ya sindano
  - Vingine – gundi, mirungi,kunusa petroli, kutumia dawa za kuondoa maumivu kinyume na matumizi yake nk.

Utumiaji Dawa Za Kulevya (Pombe, Dawa Zinginezo)

- Ipi kati ya hizi inapelekea
  - Hatari ya VVU?
  - Hatari nyinginezo?

Jinsi Ya Gani Ya Kusaidia?

- Je mtoto anatunia madawa ya kulevya?
- Je kuna tabia zingine zinazohusiana (ngono, tabia za uhalifu)?
- Je mtoto ana shauku ya kuacha kutumia dawa za kulevya?
- Tunaweza kumsaidia mtoto kuwa salama katika kutumia madawa?(kupunguza hatari)
- Je unasihi au msaada vinaweza kusaidia katika hili?

Majadiliano Na Visa Mkasa

- Maswali
- Mifano kutoka kwenye kundi
- Majadiliano

Kutatua Matatizo Ya Familia Na Watoto Walioathirika Na Kuathiriwa Ka VVU

Kutatua Matatizo:Maswala Yanayohusiana Na VVU Kwa Watoto

- Ni maswala gani ambayo wewe kama msaidizi ustawi wa jamii umekutana nayo katika kufanya kazi na walioathirika na kuathiriwa na VVU?

Bungua bongo

Maswala Yanayowaathiri Watoto Na Familia Zilizoathirika Na Kuathiriwa Na VVU

- Unyanyapaa
- Huzuni na kupotelewa kutokana na VVU
- maswala ya shule
- maswala ya kisheria
  - Kuasili na Ulinzi
  - Haki ya mali
- Kupoteza nguvu za kiuchumi na fursa
- Maswala ya afya na tiba
- Matatizo ya tabia na maswala ya afya ya akili
- Mahusiano na walezi pamoja na wanarika
- maswala ya kutoka na wapenzi
- Hasira na kutenganishwa kwenye maisha yajayo

Majukumu Ya Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Kutatua Matatizo Ya Watoto Na Familia Zilizoathirika Na Kuathiriwa Na VVU

- Kusikiliza
- Kusaidia
- Kutoa rufaa kwenda kwenye rasilimali
- Kuwaunganisha na afisa Ustawi wa Jamii na wengine wanaotoa msaada
- Kuwapa taarifa mpya zenye uhakika kuhusu VVU
- Kutatua migogoro ya dharura

Majukumu Ya Msaidizi Ustawi Wa Jamii Kama Msuluhishi Wa Matatizo

- Kusaidia kuboresha mawasiliano na wengine, m.f. wazazi,watoa huduma wengine, shule n.k.
- Kuwa kiungo cha kuboresha mahusiano
- Kutatua maswala ya unyanyasaji na kutojaliwa (mengi zaidi yataongelewa siku zijazo)
- Kusaidia kubaini iwapo familia zinaweza kutoa msaada na kama sivyo kusaidia kutafuta mbadala(mengi zaidi yataongelewasiku zijazo)
- Anza kwa kuangalia uwezo uliopo

Hata Hivyo Msaidizi Ustawi Wa Jamii Hapaswi

- Kutoa unasihi wa kina au tiba
- Kutoa matibabu au huduma zinazohusiana na afya
- Kushughulikia matatizo magumu ya kihisia yanayovuka kiwango cha mtu kupata msaada mahali pengine
- Kuyapatia ufumbuzi matatizo yote ya mtoto

Mazoezi Ya Vikundi

- Fanya kazi kwenye vikundi vya watu 7 hadi 8
- Kila kundi lifanye kazi na kisa mkasa kitakachotolewa(au kilichoundwa na wana kikundi wenyewe pamoja na muwezeshaji)
- Tambua japo hitaji moja la mtoto au familia linalohitaji unasihi
- Tambua japo njia moja ya kumsaia mtoto au familia
- Fanya Igizo dhima kuonyesha jinsi tutakavyoweza kufanya
- Jadili kile tulichojifunza na jinsi tunavyoweza kutumia kwenye visa vingine

Huduma Majumbani Kwa Watoto Wanaoishi Na Kuathiriwa Na VVU

Nini Maana Ya Huduma Majumbani?

- Jadili maana ya huduma majumbani
- Una uzoefu gani katika hili toka katika eneo unalotoka?

Huduma Za Afya Majumbani Kwa Watoto Wanaoishi Na Kuathiriwa Na VVU.

Anna ni mtoto mwenye umri wa miaka saba(7) ambaye wazazi wake wote walikufa kwa UKIMWI. Kwa sasa anaishi na bibi yake. Amekuwa mdhaifu na mwenye homa, amepimwa na kuonekana kuwa anamaambukizi ya VVU. Bibi yake anataka amuhudumie akiwa nyumbani

Wewe kama msaidizi Ustawi wa Jamii umetumwa na serikali ya manispaa kuona wana mahitaji gani na jinsi gani mtakavyo weza kuisadia familia . Unataka kuhakikisha kuwa ameunganishwa na huduma zinazohitajika.

Anna, Inaendelea

- Kaa pamoja na washiriki wengine wawili mjadili Kutegemeana na uzoefu wako katika kijiji au mji ulikotoka,ni programu gani hasa bayana za utoaji huduma majumbani zinaweza kuwa za msaada kwa Anna na bibi yake?
- Majadiliano mafupi kwenye kundi kubwa

Masuala ya Mwisho wa maisha/uhai

Masuala Ya Mwisho Wa Maisha/Uhai

- Kuwa muwazi
- Kujiandaa kwa kifo – Binafsi
- Kujiandaa kwa kifo kama mzazi
- Kuwaandaa wanafamilia wengine na marafiki kwa ajili ya kuugua kwako kwa mwisho

Kuzisaidia Familia Zinazokabiliana Na Kifo Kujiandaa Kwa Maisha Ya Baadaye: Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii

- ***Jukumu la msaidizi Ustawi wa Jamii katika kutoa msaada kwa mama***
  - Kwa ajili yake mwenyewe
  - Kumsaidia mama huyu awasiliane na watakao endelea kuwalea watoto wake
  - Kumsaidia kuwasiliana na watoto wake
    - Je ni Kwa jinsi gani umri wa watoto na mambo mengine ya msaada vinavyoweza kuathiri mchakato huu wa mawasiliano?

Je ni msaada wa aina gani anaohitaji msaidizi Ustawi wa Jamii ili aweze kutoa msaada wa aina hii?

Kuzisaidia Familia Zinazokabiliana Na Kifo Kujiandaa Kwa Maisha Ya Baadaye: Jukumu La Msaidizi Ustawi wa Jamii

- ***Jukumu la msaidizi Ustawi wa Jamii katika kuwasaidia watoto yatima***
  - Kwao binafsi na kama ndugu wa kuzaliwa nao
  - Kuwasaidia waweze kuwasiliana na atakayendele kuwalea na ndugu zake wapya
  - Kuwasaidia kuwasiliana na rafiki na wanafunzi wenzao
    - Je ni kwa jinsi gani umri wa watoto na hali zinginezo vinavyoweza kuathiri mchakato huu wa mawasiliano?

Ni msaada wa aina gani anaohitaji msaidizi Ustawi wa Jamii ili aweze kutoa msaada wa aina hii?

Muhtasari Na Mrejesho Wa Siku

Kukamilisha siku na kupongezana